# HOTUBA YA MGENI RASMI WAKATI WA SHEREHE ZA UZINDUZI WA MSIMU WA UNUNUZI WA PAMBA WA 2025/2026 KITAIFA, MWAKIBUGA, BARIADI – SIMIYU TAREHE 2 MEI, 2025

**Mhe. Shemsa Mohamed, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi-CCM Mkoa wa Simiyu;**

**Ndugu Marco Mtunga Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania;**

**Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri Balozi wa zao la Pamba;**

**Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu;**

**Katibu wa Chama cha Mapinduzi - CCM Mkoa wa Simiyu;**

**Mhe. Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Bariadi;**

**Wahe. Wakuu wa Wilaya za Busega,Bariadi,Maswa,Meatu Itilima na wakuu wa wilaya kutoka wilaya za mikoa Jirani;**

**Waheshimiwa Wabunge**

**Mhe. Destery Kiswaga, Mwenyekiti wa TCA;**

**Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Bariadi;**

**Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya za Busega,Bariadi,Maswa,Meatu Itilima**

**Wahe. Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, Busega,Maswa,Meatu Itilima;**

**Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Simiyu;**

**Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya ya Busega,Bariadi,Maswa,Meatu na Itilima;**

**Wakuu wa Idara za Kilimo na wataalam mbalimbali kutoka TCB na Mkoa wa Simiyu**

**Ndugu Watendaji Wote wa Taasisi Mbalimbali za Serikali;**

**Ndugu Wenyeviti wa Vyama Vikuu vya Ushirika;**

**Waheshimiwa wakulima wa pamba;**

**Waheshimiwa Wanunuzi wa Pamba;**

**Ndugu Wanahabari;**

**Wageni Waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana;**

**Itifaki imezingatiwa**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…**

**Ndugu wadau**

Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na nafasi ya kujumuika na wadau wa Tasnia ya Pamba hasa wakulima wa pamba wa mtaa wa **Mwakibuga** hapa wilayani **Bariadi**, wakulima na wadau wa pamba kutoka maeneo jirani na wakulima wa pamba wote nchini wanaofuatilia kupitia vyombo mbalimbali vya habari tukio hili muhimu la uzinduzi wa kitaifa wa msimu wa ununuzi wa pamba 2025/2026. Nipende pia kuushukuru uongozi wa Bodi ya Pamba kwa kunikaribisha katika sherehe hizi za uzinduzi wa msimu wa ununuzi nikiwa mgeni rasmi.

Leo ni siku ya faraja na furaha kwetu sote hapa Bariadi, Simiyu, ambapo tunakusanyika kwa ajili ya uzinduzi wa msimu wa ununuzi wa pamba wa mwaka 2025/2026. Wilaya ya Bariadi haikuchaguliwa kwa bahati mbaya; Mkoa wetu wa Simiyu ndio mkoa kinara katika uzalishaji wa pamba ambapo takribani asilimia 50 ya pamba yote inayozalishwa Tanzania inatoka mkoa wa Simiyu. Hivyo uzinduzi wa Msimu wa Ununuzi kufanyika kitaifa hapa kwetu Simiyu ni fursa ya kipekee ya kusherehekea mafanikio yetu na kuendelea kuweka mikakati thabiti ya kujiimarisha kiuchumi kupitia zao la pamba.

**Ndugu wadau,**

Uzinduzi huu unatoa nafasi kwa wakulima, wanunuzi, ushirika pamoja na viongozi wa serikali kukutana na kupata ufahamu wa pamoja juu ya masuala muhimu ya ununuzi wa pamba kabla msimu wa ununuzi haujaanza.

Ni mategemeo yangu kuwa wote mliofika hapa mtapata fursa ya kupata maelekezo/miongozo mbalimbali iliyotolewa na Serikali katika kusimamia na kuratibu soko la pamba kuhakikisha kuwa wakulima wanauza pamba kwa bei shindani na wanalipwa fedha kwa wakati.

**Ndugu wadau**

Pamba yetu ni dhahabu nyeupe, na ili iendelee kuwa na sifa ya hali ya juu katika soko la kimataifa, tunapaswa kushirikiana kuhakikisha usafi na ubora wa pamba yetu. Uchafuzi wa makusudi wa pamba unapaswa kuwa historia. Nawasihi wadau wote wakulima, wafanyabiashara, na taasisi za pamba kushikamana ili kuondoa hatari ya kupunguziwa bei katika soko la dunia kutokana na uchafuzi. Serikali kupitia Bodi ya Pamba inaendelea kutoa rai kuwepo kwa uwajibikaji na ushirikiano wa karibu kwa wadau wote wakuu kwa maana ya mkulima, vyama vya ushirika na kampuni za ununuzi

**Ndugu Wadau.**

Naomba nilisisitize jambo hili la uzingatiaji wa usafi na ubora wa pamba kwetu sote kwa kuwa kwa asilimia kubwa ya uchafu wa pamba unatokana na matendo ya makusudi ikiwemo uvunaji wa kombakomba kwa upande wa wakulima na pili ni kukosa uaminifu na uadirifu kwa baadhi ya wadau waliopewa dhamana ya kusimamia ununuzi wa pamba. Nimeambiwa kuwa hali hii ya uchafuaji wa makusudi wa pamba ilichangia kushuka kwa ubora wa pamba msimu uliopita wa 2024/2025 kutoka asilimia 44 hadi kufikia asilimia saba (7), likiwa ni anguko kubwa la madaraja ya ubora kwa miaka ya hivi karibuni.

**Ndugu Wadau**

Nimetaarifiwa kuwa katika msimu wa kilimo wa 2024/2025, serikali, kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya pamba, imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha uzalishaji wenye tija. Kupitia mradi wa **“Jenga Kesho Iliyo Bora” (BBT Ugani)** unaosimamiwa na Wizara ya Kilimo wameajiriwa maafisa ugani 740 waliopo kwenye ngazi za vijiji na kata, wanaotoa elimu ya kilimo bora cha pamba kwa karibu zaidi kwa wakulima. Maafisa hawa wanafanya kazi katika karibu asilimia 70 ya maeneo

yanayozalisha pamba nchini, na juhudi zao zimeanza kuzaa matunda.

Aidha, serikali imejipanga na mkakati wa kudumu wa kuongeza tija na uzalishaji wa pamba ili kuwasaidia wakulima kuondokana na changamoto za tija duni zinazosababishwa na upungufu wa maafisa ugani, ukosefu wa rutuba ya udongo, na mashambulizi ya wadudu waharibifu. Lengo likiwa ni kuhakikisha uzalishaji wa pamba nchini unafikia tani 1,000,000 ifikapo mwaka 2026 kama inavyoelekeza ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 – 2025. Uzalishaji huu utaifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa kwanza wa pamba barani Afrika, na hivyo kuongeza kipato cha wakulima, kuchangia uchumi wa viwanda vya nguo na mavazi, na kutoa ajira kwa wengi.

**Ndugu Wadau**

Nimefahamishwa kuwa Ili kuweza kufanikisha mkakati huu, Bodi ya Pamba imeyagawanya maeneo ya uzalishaji wa pamba katika wilaya nane za kimkakati: Maswa, Bariadi, Itilima, Meatu, Busega, Kishapu, Igunga, na Bunda, ambazo zinachangia asilimia 72 ya pamba yote nchini. Mkakati huu unajumuisha maeneo yafuatayo:

- Usambazaji wa trekta 400 kwa ajili ya kulimia kwa gharama nafuu.

- Kuandaa na kusambaza lita 7,000,000 za mbolea hai kwa ajili ya kurutubisha zao la pamba.
- Kutambulisha teknolojia za kisasa za kudhibiti wadudu, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa ndege nyuki 60, boom sprayers 300, na tractor boom sprayers 16.
- Kuajiri maafisa ugani hadi kufikia 2,000 msimu wa kilimo 2025/2026.
- Kuimarisha mtandao wa wakulima wawezeshaji na kuwapatia baiskeli wakulima wawezeshaji 2500.
- Usajili wa wakulima kidijitali ili kuimarisha mfumo wa usambazaji wa pembejeo na kudhibiti wizi na upotevu.

Hizi ni hatua za msingi zinazolenga kuleta mageuzi ya kweli katika sekta ya pamba, na nawahakikishia kuwa serikali iko tayari kuendelea kushirikiana na wadau wote ili kufanikisha malengo haya.

**Ndugu wadau**

Nimefahamishwa kwamba, katika msimu huu wa kilimo uzalishaji wa pamba unatarajiwa kufikia tani 500,000 kulinganisha na uzalishaji wa tani 149,361 za msimu wa ununuzi 2024/2026. Ongezeko ili la uzalishaji limechangiwa kwa kiasi kikubwa na

jitihada kubwa katika uwekezaji zilizofanywa kwa serikali pamoja na wadau wa tasnia ya pamba.

**Wadau wa Pamba**

Serikali imekuwa na nia ya dhati kuimarisha mfumo mzima wa uendeshaji wa ushirika nchini kama tulivyoshuhudia hivi karibuni ambapo Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua benki ya Ushirika yenye lengo la kukuza mitaji ya vyama vya ushirika viweze kujiendesha kwa ufanisi. Nia hii ya dhati ya Muheshimiwa Rais inatutaka sisi tulio katika ngazi mbalimbali za utendaji kutekeleza ipasavyo majukumu yetu kwa uaminifu na uadirifu mkubwa.

**Ndugu Wadau**

Kama nilivyotangulia kusema awali kuhusiana na kushuka kwa ubora wa pamba nchini mnaweza kukubaliana nami kuwa endapo tutamuunga mkono Mheshimiwa Rais na nia yake ya kuimarisha ushirika basi naamini tatizo la uchafu na kushuka kwa ubora wa pamba litakuwa historia na kuifanya pamba yetu inunuliwe kwa bei nzuri katika soko. Aidha azma hii ya Mheshimiwa Rais kuona kama nchi tunakuwa na mfumo imara wa Ushirika inaoneshwa pia na kuendelea kwa uendeshaji wa ununuzi wa pamba msimu wa 2025/2026 kupitia mfumo wa vyama vya msingi vya ushirika

yaani **AMCOS model**. Natoa rai kwa wana ushirika tusimuangushe Mheshimiwa Rais wetu kwa Imani hii kubwa aliyoionesha kwetu kwa kuhakikisha kuwa tunasimamia vema ununuzi wa haki kwa pande zote mbili (mnunuzi na mkulima) na tunalinda kwa kila hali usafi na ubora wa pamba.

**Ndugu Wadau**

Nimejulishwa kuwa katika msimu wa ununuzi 2025/2026 shilingi tano (5) itachangiwa na wanunuzi kwa ajili ya kugharamia usimamizi wa usafi na ubora katika vituo vyote vya ununuzi wa pamba. Ushuru huu unapaswa kulipwa kwa wakati na kampuni zote za ununuzi wa pamba ili kuwezesha usimamizi wa uzingatiaji wa usafi na ubora wa pamba. Aidha haki lazima iende sambamba na wajibu hivyo nazihasa AMCOS ambazo zina dhamana ya kununua pamba katika kusimamia misingi ya haki na kuhakikisha uzingatiaji wa usafi na ubora kabla pamba haijafika mnunuzi zitimize wajibu wao ipasavyo katika shughuli ya usimamizi wa usafi na ubora.

**Ndugu Wadau**

Niwaombe viongozi wenzangu katika mikoa inayolima pamba kwamba, wakaguzi wa pamba wa Bodi ya Pamba ni wachache, hawawezi kufika kila eneo (gulio la kununulia pamba) kwa muda

muafaka. Zao hili ni letu sote na hatuwezi kufumbia macho matendo ambayo yanadidimiza kilimo cha pamba hususan katika mkoa wangu wa Simiyu.

Viongozi wenzangu katika mikoa mingine, ninachukua fursa hii kuwaomba tuwaagize wasaidizi wetu walisimamie suala hili na Halmashauri ziwasaidie wakulima wa pamba kuboresha uzalishaji, kwa uchafuzi wa pamba unafika mwisho badala ya kujikita tu katika kukusanya ushuru tu. Tutambue kuwa uzalishaji wa mazao ukiongezeka ushuru nao pia utaongezeka.

**Ndugu Wadau**

Katika ununuzi wa pamba kwa misimu kadhaa pamekuwa na malalamiko ya wakulima kuwa baadhi ya watendaji wasio waaminifu kuwapunja uzito wakati wa kupima pamba kwa kuchezea mizani ya kupimia pamba na kunyonya jasho la mkulima ambae kapambana kwa kipindi kirefu kuzalisha. Serikali ya awamu ya sita imekuwa ikisimamia ufanyikaji biashara kwa usawa kama vile kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mizani kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) sambamba na kuchukua hatua kali za kisheria kwa wale wote wanaothibitika kwa kukutwa na hatia ya uchezeshaji mizani. Ikiwa kama njia mojawapo ya kukabiliana na tatizo hili nimetaarifiwa kuwa leo hii Bodi ya Pamba itazindua **Mizani Janja** ambayo ni mizani ya kisasa

iliyoboreshwa itakayotatua kwa kiasi kikubwa changamoto na kuziba mianya ya mkulima kupunjwa anapoenda kuuza pamba. Aidha kutambulishwa kwa matumizi ya Mizani Janja katika tasnia ya pamba kutawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za uzalishaji wa pamba nchini na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa ushuru kwa Halmashauri zetu unaowezesha ustawi wa jamii katika maeneo yanayozalisha pamba. Katika hatua za awali Mizani Janja itaanza kutumika msimu 2025/2026 kwenye wilaya saba za Kimkakati zikiwemo wilaya zote za mkoa wa Simiyu za Bariadi, Busega, Itilima, Maswa, na Meatu wilaya nyingine ni Igunga mkoa wa Tabora na Tanganyika mkoa wa Katavi.

**Ndugu wadau,**

Baada ya maelezo haya machache, napenda kutumia nafasi hii kutamka rasmi kuwa msimu wa ununuzi wa pamba **2025/2026** sasa umefunguliwa rasmi na bei elekezi ya pamba msimu huu wa ununuzi ni shilingi **Elfu Moja na mia hamsini (1,150/=)** kwa pamba **Daraja A** na shilingi mia tano na sabini na tano **575/=** kwa pamba **Daraja B** na mnunuzi hataruhusiwa kununua chini ya bei hii.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**